

# Pambazuko

Toleo Namba 0042

Jumatatu Julai 17-23, 2023



## Jaribio kubwa kwa Rais Samia

Uk. 7

● *Wananchi waonya kiongozi wa nchi kubagazwa, kutukanwa*

**Hoja, maswali, majibu kuhusu Bandari**

**Uk. 5/6**

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Msimamo

## Mhimili wa Pambazuko

**G**AZETI la Pambazuko linandelea kujenga heshima kwa kuwapa wasomaji wake habari ambazo zimefanyiwa kazi kwa kina na zenye kubeba taswira ya haki kwa manufaa na neema ya Tanzania na dunia.

Pambazuko limekuwa gazeti la mfano na rejea mahali pengi tangu kuanzishwa kwake mwaka jana na linaendelea kujiimarisha kitaaluma kadri inavyowezekana.

Ni kutokana na imani kutoka kwa wasomaji wake, tumeona ni vyema kuweka kwa umma misingi na imani za waandishi wa habari wa Pambazuko ili kila msomaji atambue kuwa watendaji wa Pambazuko wanasimama katika imani za namna gani.

Watu wengi wameuliza, je, Pambazuko ni gazeti kama magazeti mengine, mbona halionekani mitaani – kwenye meza za kuuza magazeti na linajipambanua kuwa tofauti na magazeti mengine, kuanzia aina ya uandishi wake, namna linavyosambazwa na matumizi ya lugha fasaha?

Jibu la swali hili ni rahisi kwa maana kwamba waandishi wa habari wa Pambazuko ni wanataaluma ambao wanasimamia misingi na weledi katika kuchakata habari, lakini pia wanasimamia imani 10 ambazo zimekuwa mwongozo wa utendaji wao wa kila siku.

Pamoja na kwamba gazeti hili husambazwa bure kwa njia ya WhatsApp na emaili, ni chombo ambacho kimesajiliwa na kutambuliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa pande zote mbili; Tanzania Bara na Zanzibar.

Hivyo, ni chombo cha habari chenye hadhi sawa na magazeti,

redio, vituo vya televisheni na vyombo vingine rasmi na vinavyotambulika.

Imani 10 za mwandishi wa Pambazuko

1. Kwamba kufikiri na kuamua kwa uwazi, usahihi na kuandika habari kwa kuzingatia miiko ya uandishi wa habari ndiyo msingi wa kazi zangu.

2. Kwamba kamwe sitaandika habari za kutunga, uongo wala uzandiki kwa lengo la kudanganya jamii au kuumiza yeyote.

3. Kwamba nitahakikisha kinachopeleka kwa mhariri ni ukweli, tena ukweli mtupu.

4. Kwamba nitaweza kuitetea – kwa ushahidi, habari ambayo nitaandika hata ikiwa ni mahakamani.

5. Kwamba nitashiriki kuhakikisha matangazo, habari, makala, safu na hata barua za wasomaji zinazingatia miiko ya uandishi wa habari na kamwe hazina lengo lililojificha wala kuzua taharuki.

6. Kwamba ubora wa kazi zangu – kupitia Pambazuko, utapimwa kwa uadilifu, uaminifu na usahihi wa kile kinachochapisha.

7. Kwamba, kumcha Mungu ni chanzo cha maarifa na uandishi bora, elimu bora; darasani na chumba cha habari cha Pambazuko, ni sehemu muhimu kujiendeleza kitaaluma.

8. Kwamba sitaogopa kuandika ukweli, hata kama utaumiza baadhi ya watu. Lengo ni kuponya jamii pana.

9. Kwamba rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea na nitaandika wanaojihusisha nayo ili kuokoa jamii.

10. Ninaamini kuwa uandishi bora wa habari siku zote unajali utu, kamwe sitabagua.

## **SALUTI KWAKO MKUU...**



*Jumapili ya Julai 9, 2023 kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francisco alimteua Askofu Mkuu Mwandamizi Jimbo Kuu la Tabora, Protase Rugambwa kuwa kardinali nchini Tanzania. Katika picha hii Papa akiwa na Rugambwa katika moja ya shughuli za kanisa hilo. Gazeti la Pambazuko linampongeza Askofu Mkuu Mwandamizi Rugambwa kwa kuaminiwa na Kanisa na tuna amini kwamba anakwenda kutenda vyema na haki kwenye nafasi hiyo mpya baada ya kuapishwa.*

### **Jisajili kupata Pambazuko bure**

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

### **NUKUU**



*“Tunafanya kila tuwezalo kuwapa elimu, lakini uamuzi wa kuitumia elimu hiyo ni wenu, tambueni kuwa upo mzigo mkubwa sana wa kuongoza hii nchi unawasubiri, someni kwa bidii sana, msituangushe, na zaidi sana msipate ukimwi” -*

*Benjamin Mkapa, Rais wa Tanzania (1995-2005).*

## Tafakuri

## Mkatamba Bandari wasaidia kutambuana

Na Askofu Dkt Stephen MUNGA

**Z**AIDI ya mwezi mmoja sasa, vyombo yakiwamo makundi ya WhatsApp, Twitter na majukwaa mengine, yamejaa kinachoweza kuitwa minyukano ya hoja kwa kutetea au “kuponda” Mkatamba wa Kiserikali (IGA) – kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Emirati ya Dubai.

Mkatamba wa serikali hizo mbili uliosainiwa na wawakilishi wa serikali hizo na baadaye kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Juni 10, 2023 unahusu Ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii kwa Maendeleo na Kuimarisha Utendaji wa Bandari za Bahari na Maziwa Tanzania.

Hadi sasa serikali imekuwa na msimamo wake, wananchi nao wapo wanaoona mkatamba huo ni mzuri mno, wengine wakiwa na mawazo tofauti. Kimsingi, hakuna makubaliano ya jumla; kwamba unafaa ama haufai na unahitaji marekebisho kadhaa.

“Na hivi ndivyo tunavyoweza kutambua wazi kati ya walio watoto wa Mungu na walio watoto wa shetani. Mtu ye yote asiyetenda lililo haki si wa Mungu; wala asiyempenda ndugu yake si wa Mungu.” - (1 Yohana 3:10)

**Kwanza**, ninakubaliana na mtazamo kuwa ndugu hujuaana vizuri wakati wa matatizo na migogoro. Hata uliodhani wanakuheshimu utawasikia wakikutukana. Wasio tahili kutukana walijaribu kuvunja heshima hata watu wanaoaminiwa na dunia nzima kutokana na weledi wao. Heshima zao hazivunjwi

kirahisi kutokana na misimamo yao.

Pili, huo unaoonekana sasa kuwa mgogoro wa bandari, umetufanya tujuane vizuri Watanzania. Baadhi ya watu walitiwa kiza, ufahamu na adabu zao sasa zimedhihiri kwamba hawakuwa nazo – muda huu wanaonekana kama waliosimama uchi hadharani. Tukumbuke kuwa kujaribu kufunika ukweli na kufukia haki ni kama kuzima moto kwa petroli.

**Tatu**, uzalendo na maadili mema tunayoendelea kuyaweka katika misingi imara, kamwe tusipoteze kwa kuwa tunapata hiki ama kile. Tuweke utaiifa wetu mbele na hakika dunia itatuheshimu kwa misimamo yetu – kwa kuwa tumetenda haki kwa umma na hasa ule wa vizazi vinavyokuja.

Katika kipindi hiki, tumeshuhudia hata viongozi wa dini wenye dhamana ya kuadibisha jamii, wametumika kwa uongo na majungu. Sasa utamwambiaje mtoto asitukane wakati mwenyewe ni mtukanaji. Tusiwarahibie watoto maisha kwa ajili ya ulafi wa leo.

Nne, tumedhalilishana kwa hoja zisizo na ufahamu wa kina. Wapo watu ambao akipewa kipande cha mkate aweza kutukana kijiji kizima. Hekima ni pamoja na kujua la kuzungumza kwa wakati ufao na kwa kiasi kifaacho.

Tuelewe kuwa hivi ni vita vikubwa kwani ni mvutano baina ya kweli na uongo; haki na dhuluma; wema na uovu; giza na nuru; na uzalendo na usaliti. Mpaka tutakapofika mwisho tutakuwa tumejuana vizuri. Kwamba asiyetenda lililo haki si wa Mungu; wala asiyempenda ndugu yake si wa Mungu.



## **Serikali yajibu maswali Mkataba Bandari**

**I**JUMAA ya wiki iliyopita - Julai 14, Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) liliandaa mkutano wa wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari na kuwakutanisha na watendaji wakuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, wakiongozwa na waziri wake, Prof. Makame Mnyaa Mbarawa.

Katika mkutano huo uliorushwa mbashara na vituo karibu vyote vya televisheni na mitandao ya kijamii, maswali mengi, dukuduku na hoja mbalimbali zilitolewa na kupewa ufafanuzi na wataalamu wa wizara hiyo, wakiongozwa na Hamza Johari – mbobezi katika mikataba ya kiataifa, ambaye alikuwa mwenyekiti wa kamati ya majadiliano ya mkataba unaojadiliwa.

Miongoni mwa watendaji wa wizara hiyo, walikuwamo wanasheria, wataalamu wa mikataba ya kimataifa na pia mwenyekiti wa kamati ya majadiliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Emirati ya Dubai kuhusu mkataba wa ushirikiano, ambao sehemu kubwa unahusu kujodishwa kwa baadhi ya bandari za Tanzania kwa kampuni ya Dp World ya Dubai ili kuendesha bandari hizo.

Maswali mengi yaliulizwa, lakini gazeti hili la Pambazuko linakuletea baadhi ili kupata msimamo wa serikali katika “sintofahamu” hii ya mkataba huo ambao Julai 10, 2023, Bunge la Jamhuri ya Muungano liliuridhia.

Pamoja na ukweli kwamba ipo sintofahamu katika mkataba huo, lakini wote wanaouzungumzia, wanakiri kwamba upo umuhimu wa kuwa na mwekezaji makini ili Tanzania ijihakikishie inapata mapato makubwa kupitia bandari zake.

Yafuatayo ni baadhi ya maswali hayo na majibu yake kutoka serikalini;

**Je, Dubai inaruhusiwa kuingia mkataba na Tanzania?**

Jibu ni ndiyo. Pamoja na kwamba Dubai ni sehemu ya Muungano wa Falme za Kiarabu (UAE), suala la uwekezaji siyo sehemu ya masuala ya Muungano huo. Katiba ya UAE imeeleza kuhusu masuala



*Prof Mbarawa*

ya Muungano na yasiyokuwamo, suala la uwekezaji halimo.

**Je, mapendekezo ya kuboresha mkataba yanayotolewa sasa yatafanyiwa kazi?**

Ndiyo. Makubaliano ya Tanzania na Dubai yametoa fursa ya kufanya marekebisho kwenye mikataba ya kibiashara ambayo itafuata. Lakini hatua hiyo itafuata baada ya mkataba kuridhiwa kwenye mabunge ya nchi hizo na taratibu za mabadilishano ya nyaraka baina ya pande mbili (exchange of instruments) kukamilika.

**Je, wanaokosoa mkataba ulioingiwa baina ya serikali za Tanzania na Dubai (IGA) wana hoja?**

Nyingi ya hoja zinazotolewa – karibu hoja nane kati ya kila 10, hazihusu IGA, bali mikataba mahsusi ya kibiashara na hata kijamii itakayoingiwa wakati wa utekelezaji wa makubaliano ya Tanzania na Dubai. Kwa mfano, masuala kama ukomo wa mkataba, kiwango cha uwekezaji, idadi ya ajira na mambo mengi yanayozungumzwa yatafanyiwa kazi kwenye mikataba itakayoingiwa baadaye.

**Je, kuna maelezo kuwa mkataba unatoa wajibu kwa Tanzania na haki kwa Dubai. Kuna ukweli?**

Dhana ya IGA ni mpya. Kuna tofauti

## Mkataba

## Serikali yajibu maswali Mkataba Bandari

*Inatoka Uk. 5*

kati ya IGA na mikataba ya biashara baina ya nchi na nchi (BIT). Mkataba huu wa sasa, unahusu uwekezaji unaofanyika Tanzania na siyo biashara baina ya Tanzania na Dubai. Katika IGA, hili ni la kawaida kwa sababu Tanzania ndiyo mwenyeji na uwekezaji wote utafanyika kwake. Ni muhimu haki za anayeleta mtaji zikazingatiwa.

**Je, mkataba unauza bandari zetu?**

Hapana. Kimsingi, mkataba unahusu uendeshaji ambao ni asilimia nane tu ya shughuli zote za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Kwa miaka 22 iliyopita, kampuni ya TICTS ilikuwa ikifanya shughuli kama hizo na bandari yetu- ya Dar es Salaam haikuwa imezwa au kubinafsishwa.

**Je, Watanzania watapoteza ajira baada ya ujio wa DP World?**

Hapana. Suala la ajira kwa Watanzania limewekwa kifungu kabisa kwenye IGA. Hakuna mfanyakazi hata mmoja wa Bandari ambaye atapoteza ajira kutokana na shughuli za uendeshaji baada ya DP World kuanza.

Inatarajiwa kuwa ufanisi na ubora wa huduma utakoaanza, utasababisha kuwapo kwa ajira nyingi zaidi kuliko ilivyo sasa, hata kama mwekezaji atakuja na teknolojia kubwa yenye ufanisi na usasa.

**Je, DP World itauziwa ardhi ya Tanzania?**

Hakuna ardhi ambayo DP World itauziwa kwa mujibu wa mkataba uliopo. TICTS haikuuziwa ardhi yoyote ya Tanzania kwa miaka yote iliyokuwa ikiendesha shughuli za makasha (makontena) kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

**Je, uwekezaji utaathiri ulinzi na usalama wa Tanzania?**

Hapana. Kama ilivyo viwanja vya ndege, Bandari ya Dar es Salaam pia ni lango la kuingilia Tanzania. Kwa sasa, viwanja vya ndege kuna watoa huduma kama Swissport na wengine na bado



*Mkuurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)- Hamsa Johari*

vyombo vya ulinzi na usalama vinaendelea na majukumu yake kama kawaida.

Suala la ulinzi kwenye maeneo nyeti ya nchi yetu litabaki kuwa jukumu la vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

**Je, kwanini serikali haiwekezi yenyewe na inaita wageni?**

Uzoefu duniani kote unaonyesha sekta binafsi ni mahiri zaidi katika uendeshaji wa shughuli za bandari kuliko serikali. Nchi nyingi duniani, wakiwamo jirani zetu kama Kenya, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini, Angola, Ghana na kwingine bandari zinaendesha na sekta binafsi.

Pia, DP World ina meli takribani 400 na maana yake ni kwamba kuwa nao kunahakikisha biashara ya uhakika kwa sababu ya mtandao mpana ilionao kampuni hiyo na kwamba wao wenyewe ni watafutaji wa masoko ya bidhaa zinazotakiwa kusafirishwa.

**Kwanini uwekezaji huu ni muhimu?**

Uwekezaji huu unatarajiwa kuongeza mchango wa sekta ya bandari kwenye mapato ya nchi kutoka asilimia 37 za sasa hadi takribani asilimia 70.

Jambo hili litaipe serikali uwezo mkubwa zaidi wa kusaidia sekta muhimu kwa jamii kama vile elimu, afya, maji na kuzimua sekta nyingine za uchumi na hivyo kuchochea upatikanaji wa ajira kwa watu wengi zaidi na kuchangia nguvu kwenye matamanio ya serikali kupunguza umasikini kwa kiasi kikubwa.

## Jaribio kwa Rais Samia

Na Tryruckia MFINANGA

**I**DADI kubwa ya wananchi wa Tanzania hawapendezwi na tabia inayoonekana “kuota mizizi” sasa; ya kubeza, kudharau, kubagaza na hata kutukana viongozi wakuu wa nchi, akiwamo Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Ulinzi na Usalama, Samia Suluhu Hassan.

Katika kipindi cha mwezi mmoja; kuanzia Juni 12, hadi Julai 11, gazeti la Pambazuko lilifanya kazi ya kupitia baadhi ya mitandao ya jamii, televisheni mtandao, kuzungumza na watu wa kada mbalimbali, kuhusu maoni yao na namna wanavyopokea kejeli na hata matusi kwa viongozi wakuu wa Tanzania; rais, makamu wake na waziri mkuu.

Ndani ya muda huo, Pambazuko limebaini kwamba katika makundi ya WhatsApp, mtandao wa Twitter na televisheni mtandao, kiongozi “aliyeporomoshewa” matusi, kejeli, kubezwa na kubagazwa ni Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwamba katika kipindi hicho, baadhi ya watu wenye majina bandia, wakitumia mitandao ya kijamii, walibeza, kukejeli na kumbagaza Rais Samia binafsi kwa kumuita majina yasiyofaa na yasiyokuwa na ustaarabu wa Mtanzania.

Pia wapo baadhi ya wananchi waliotumia televisheni mtandao kujirekodi ama kurekodiwa kwenye mtandao wa Youtube ambako wanaonekana na kusikia wakitamka maneno mabaya dhidi ya viongozi hao wakuu wa Tanzania.

Pambazuko limebaini kuwa katika kipindi hiki cha malumbano kuhusu faida na ama hofu ya kuwa na mwekezaji kutoka Emirati ya Dubai – DP World ambaye anawekeza kwenye kusimamia na kuendesha baadhi ya bandari za Tanzania, matusi yameongezeka ikilinganishwa na kipindi chochote tangu kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Sita, ikiongozwa na Rais Samia.

Pambazuko haliwezi kuyaandika matusi hayo kulingana na sera yake ya



**Rais Samia**

uhariri na staha ya Mtanzania, isipokuwa linaweza kueleza kwamba miongoni mwa walioongoza kukejeli, kutusi ni pamoja na wanasheria na baadhi ya wanaojitua wanaharakati.

Akizungumza na Pambazuko, mkazi wa Mwenge, Dar es Salaam, Hamduni Hamis anasema kwamba siyo vyema kwa kiongozi wa nchi kutukanwa popote, kwani hatua hiyo ni kuvunja heshima na misingi ya utu.

“Hivi karibuni nimeona na nimekuwa nikisoma, hasa kwenye mitandao ya kijamii, rais akitukanwa, hii siyo sawa na haikubaliki kwetu,” anaongeza Hamduni.

Mwalimu mstaafu, Simon Kulanga anayeishi Ngudu, Kwimba, Mwanza anasema kwamba tabia ya kutusi viongozi, hata kama baadhi ya uamuzi wao unaonekana kutofautiana na baadhi ya watu, haipendezi na anawaomba Watanzania “kuacha mara moja” tabia hiyo.

Conrad Mageta wa Kahangara, Magu, Mwanza anasema kwamba ameshangazwa kusoma na kusikia viongozi wakuu wa Tanzania wakifanyiwa dhihaka na kebehi kupitia mitandao ya kijamii na kuonya kwamba “tabia hiyo haifai.”

Tayari serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, imetoa onyo kwa wote wanaotumia mitandao ya kijamii vibaya kutusi viongozi na kuwataka wanaofanya hivyo kuacha haraka, vinginevyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.



## Wanasheria

### TLS yahadhari, yatoa ushauri Mkatamba Bandari

**C**HAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kimefanya mapitio, kuchambua na kutoa maoni yake juu ya mkataba wa serikali kwa serikali (IGA) ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Emirari ya Dubai umefungwa.

Mkatamba huo wa ushirikiano, umejikita zaidi katika uendeshaji wa bandari za Tanzania, ambapo kampuni ya DP World itakuwa na jukumu la kuendesha na kusimamia baadhi ya bandari za bahari na maziwa ya Tanzania.

TLS inatambua na inakubali juhudi nzuri za serikali za kuwavutia wawekezaji wa kigeni na kuchochea uchumi wa taifa kwa faida ya ustawi wa nchi. TLS inaunga mkono kabisa juhudi zote zinazoboresha ustawi wa taifa, utawala wa sheria.

Walakini, TLS inasihi Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha ushiriki wa umma wa kutosha na kwa kina katika hatua za kupanga, kujadili, na kufanya uamuzi kuhusu rasilimali za taifa na uwekezaji wa aina hiyo kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haswa Ibara 8 na 9, na haswa, Ibara 21 (2), ambayo inampa kila raia haki na uhuru wa kushiriki kikamilifu katika mchakato unaosababisha uamuzi juu ya masuala yanayomhusu yeye, ustawi wake au taifa.

TLS inaona kuwa Mkatamba wa Serikali kwa Serikali (IGA) haukufanyiwa kazi vizuri, kusababisha utata, shaka, utata na tafsiri tofauti na wahusika tofauti. Pia, kuna vipengele / vifungu vinavyopuza, kinyume au kinyume na maslahi ya taifa, na tunapendekeza kuondolewa kabisa.

Vifungu hivi vinaweza kusababisha migogoro wakati wa utekelezaji wa IGA, HGAs inayofuata, na Mikataba ya Mradi. Kwa hivyo, TLS inapigania ushiriki wa wataalam na wadau wenye ujuzi maalum kushiriki maoni yao juu ya masuala muhimu kuelekea kurekebisha vipengele



Rais wa TLS Harold Sungusia

vilivyotajwa.

Tunasisitiza umuhimu wa kutumia wataalamu wa TLS na/ au mawakili binafsi kusaidia taifa letu katika mazungumzo na uandishi wa makubaliano muhimu ya uwekezaji, kuhakikisha uwazi bora, ufanisi, na kupunguza hatari za migogoro ya uwekezaji ya baadaye, ambayo inaweza kuwa ghali kwa nchi yetu.

Zaidi ya hayo, tunapendekeza sana, tunapendekeza sana marekebesho makubwa kwa mfumo wa kisheria wa Tanzania kuhusu taratibu za kuidhinisha makubaliano ya kimataifa. Kanuni za Bunge (Juni 2020) kifungu cha 108 kinapaswa kurekebishwa ili kuimarisha jukumu la Bunge katika taratibu za idhini. TLS inaomba Kanuni za Bunge zirekebishwe ili kuagiza muda wa kutosha ambao wadau wanaweza kuchambua makubaliano kwa kina na kuwasilisha mapendekezo yao kwa Kamati za Bunge



## **TLS yahadhari, yatoa ushauri Mkataba Bandari**

husika.

**2. MAONI YA KITEKNI YA TLS  
KUHUSU MAKUBALIANO YA  
KISERIKALI-KISERIKALI (IGA)**

**2.1. MAENEO YA USHIRIKIANO  
YALIYO KIHALALI**

2.1.1. Kifungu: Kifungu cha 2 cha IGA kinathibitisha mfumo halali wa maeneo ya ushirikiano unazingatia maendeleo, uboreshaji, usimamizi, na uendeshaji wa bandari za baharini na za ziwa, maeneo maalum ya kiuchumi, mbuga za vifaa, njia za biashara, na miundombinu mingine inayohusiana na bandari.

Pia inajumuisha maeneo kama ujenzi wa uwezo, uhamishaji wa maarifa, maendeleo ya ujuzi, uhamishaji wa teknolojia, kuimarisha taasisi za mafunzo, na kusaidia uwezo wa soko.

2.1.2. Uchunguzi wa TLS: Baadhi ya wadau, kama ilivyobainishwa na TLS, wanaamini kuwa Kifungu cha 2 cha IGA kinamaanisha kuwa Tanzania imezuiliwa kufanya mazungumzo na vyama vingine kuhusu maendeleo ya bandari kwenye pwani ya Bahari ya Hindi na Ziwa Tanganyika, Victoria, Nyasa, na vinginevyo.

Tafsiri hii imepelekea baadhi ya wananchi na wadau kuamini kuwa kifungu hiki kinazuia uwezo wa Tanzania kushirikiana na vyama vingine.

2.1.3. Mapendekezo ya TLS: TLS inapendekeza kwamba vipengele vya IGA vizingatiwe kwa pamoja. Katika muktadha huu, Kifungu cha 2, kusomwa pamoja na Kifungu cha 4 (2) na Kifungu cha 5 (1) cha IGA, kinatoa haki ya pekee kwa DP World kuhusiana na miradi iliyoainishwa chini ya Kiambatisho-1 Awamu ya 1.

Zaidi ya hayo, haki hiyo ya pekee inakwisha baada ya miezi 12 tangu tarehe ya saini ya IGA, ikiwa DPW au washirika wake watatofautiana na Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA) ndani ya miezi 12 au kushindwa kufanya hivyo, chochote

kitakachotokea mapema. Kuhusu miradi ambayo haijatajwa katika Kiambatisho-1 Awamu ya 1, hakuna haki ya pekee, na Tanzania ina haki ya kushirikiana na wawekezaji wengine zaidi ya DP World.

Tafsiri hii inalingana na jukumu la Kifungu cha 4 (2) kwa Tanzania kuwajulisha Dubai juu ya fursa nyingine (labda katika Kiambatisho-1 Awamu ya 2) zinazohusiana na maeneo huru na sekta za vifaa nchini Tanzania, kuruhusu vyombo vya Dubai kutoa maslahi na kuwasilisha mapendekezo.

TLS inapendekeza Kifungu cha 2 kurekebishwa kwa uwazi, kwa kusema kuwa maeneo yaliyoelezwa hayako pekee kwa DPW isipokuwa kwa miradi iliyoorodheshwa katika Kiambatisho-1 Awamu ya 1. Hii itahakikisha maana kamili ya Kifungu cha 2 inaeleweka bila kurejelea Kifungu cha 5 (1) na 4 (2) cha IGA.

2.1.4 Msingi wa Mapendekezo ya TLS: Kwa sasa, Kifungu cha 2 cha IGA kinaweza kutafsiriwa kwa upana, na hivyo kudhuru maslahi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kifungu cha 9(j) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinahitaji shughuli za kiuchumi zisababisha umiliki wa utajiri au ukiritimba wa njia muhimu za uzalishaji mikononi mwa wachache.

2.1.5. Athari Inayotarajiwa ya Tatizo kwa Nchi Yetu: Ikiwa kifungu hiki kitabaki bila kufanyiwa marekebisho, kinaweza kusababisha tafsiri tofauti kwa kila upande, na hivyo kusababisha migogoro ya biashara/ uwekezaji. Ikiwa DP World itachukua tafsiri pana, IGA inaweza kusababisha athari mbaya zisizotarajiwa kwa bandari nyingine ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### **2.2. UFUMBULIAJI WA MIGOGORO**

2.2.1. Kifungu: Kifungu cha 20 kinatoa mfumo wa ufumbuzi wa migogoro kupitia usuluhishi.

## Wanasheria

### TLS yahadhari, yatoa ushauri

*Inatoka Uk. 9*

2.2.2. Uchunguzi wa TLS: TLS inaamini kuwa mchakato wa usuluhishi uliowekwa katika Kifungu cha 20 cha IGA ni mrefu. Vifungu katika Kifungu cha 20 vinabainisha kuwa migogoro yoyote inayohusiana na IGA inapaswa kutatuliwa kwa njia ya amani na pande husika, au kupitia Kamati ya Mashauriano ya IGA iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 3 cha IGA.

Ikiwa mgogoro hautatuliwa ndani ya siku 90, upande ulioathirika unaweza kutangaza mgogoro, baada ya hapo mchakato wa kuteua wasuluhishi na mwenyekiti huanza. Mchakato wa uteuzi pekee unaweza kuchukua hadi siku 90 ikiwa wasuluhishi wawili hawakubaliani kuhusu wasuluhishi wa tatu, ambaye atakuwa mwenyekiti, na hivyo kuhitaji kurejelewa kwa Katibu Mkuu wa Mahakama ya Usuluhishi wa Kudumu iliyoko The Hague.

2.2.3. Mapendekezo ya TLS: Kipindi kabla ya kuomba usuluhishi ni kirefu sana. Pande husika zinapaswa kuzingatia kupunguza kipindi hiki kabla ya kuanza mchakato wa ufumbuzi wa migogoro. TLS inapendekeza kuwa kipindi cha ufumbuzi wa amani na kipindi kabla ya kuomba usuluhishi kabla ya kuanza mchakato wa ufumbuzi wa migogoro kisizidi siku 90.

2.2.4. Msingi wa Mapendekezo: TLS inaashiria uamuzi katika Kesi ya Mzalishaji dhidi ya Mzalishaji, Tuzo ya Mwisho, ICC Kesi Namba 8445, 1994, ambapo ilisemwa kuwa:—"Wasuluhishi wanaamini kuwa kifungu kinachotaka kujaribu kutatua mgogoro kwa njia ya amani ni kielelezo cha nia, na kinapaswa kutazamwa kwa muktadha.

Hawapaswi kutumika kwa njia ambayo inawalazimisha pande kujihusisha katika mazungumzo yasiyo na tija au kuchelewesha ufumbuzi wa utaratibu wa mgogoro. Kwa hivyo, wasuluhishi wameamua kuwa hakukuwa na wajibu kwa mlalamikaji kufanya juhudi zaidi za kupata suluhisho la amani, na kwamba

kuanza kwa mchakato huu wa usuluhishi haukuwa mapema au batili.

2.2.5. Athari Inayotarajiwa ya Tatizo kwa Nchi Yetu: Ikiwa kifungu hiki kitabaki bila kufanyiwa marekebisho, kinaweza kusababisha mchakato mrefu wa ufumbuzi wa migogoro. Wakati huo huo, upande unaopingana unaweza kuendelea na shughuli za biashara wakati wa kipindi hiki kirefu, na hivyo kudhuru maslahi ya upande ulioathirika. Tanzania inapaswa kuepuka utaratibu wowote wa kutatua migogoro ambao unaweza kuchelewesha au kusababisha mazungumzo yasiyo na tija.

#### 2.3 SHERIA INAYOONGOZA MKATABA

2.3.1. Kifungu cha 21 cha IGA kinaeleza vipengele vya sheria inayoongoza. IGA inabainisha kuwa inaongozwa na Sheria ya Kiingereza, wakati Mkataba wa Serikali Mwenyeji (HGAs) na Mkataba wa Mradi unaongozwa na sheria za Tanzania.

Kwa wakati mmoja, Kifungu cha 25 (3) kinaeleza kuwa vipengele vya IGA vitatumika kwa shughuli zote za Mradi kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 1, ikiwa ni pamoja na zile zilizofanywa kabla ya IGA au HGAs husika kuanza kutumika. Kifungu cha 17 kinataka haki za wafanyakazi na afya ya kazi zinaongozwa na sheria za Tanzania, na Kifungu cha 18 kinataka kodi, ada, na ushuru unaongozwa na sheria za Tanzania.

2.3.2. Uchunguzi wa TLS: TLS inaona kuwa Kifungu cha 21 kinatoa sheria inayopingana (Sheria ya Kiingereza dhidi ya Sheria ya Tanzania). Kwa mfano, ni kawaida kuwa na mikataba ya mkopo inayoongozwa na sheria nyingine isipokuwa sheria ya Tanzania, lakini ni vigumu kutumia sheria ya Kiingereza kwa masuala ya haki za ardhi, motisha za uwekezaji, masuala ya mazingira na afya ya kazi, haki za usalama na



***Epuka magonjwa, kunywa maziwa ya mbuzi***



**K**ila mtu ni mwamuzi wa afya yake, lakini kwanaoamua kunywa maziwa ya mbuzi, wanaweza kujihakikishia uimara wa afya zao, familia, ndugu na jamaa.

Kitonga farm, shamba la mifugo linazalisha maziwa halisi ya mbuzi ambayo yanapatikana Bunju, Dar es Salaam na mteja anaweza kuletewa alipo ndani ya jiji hilo.

Faida za maziwa ya mbuzi ambazo zimethibitishwa na wataalamu wa lische na tiba ni pamoja na changamoto za afya ziafuatazo:

Hupambana na uvimbe(mwako) katika mwili wa binadamu. Huzuia na kuondoa uvimbe unaoanza kumea

Ni chanzo muhimu katika kuchakata madini mwilini; madini chuma(Fe) na shaba(Cu) hasa kwa watu wenye matatizo ya mfumo wa umengenyaji.

Maziwa ya mbuzi yana molekuli ndogo za mafuta kuliko zile zilizoamo katika mafuta ya wanyama wengine, hivyo kuwa chachu ya kuepusha magonjwa mengi

Njoo Kitonga House of Milk, iiyoko Barabara ya Bunju Beach, kuelekea Shule ya Moha uimarisha afya kwa kunywa maziwa ya mbuzi, huku ukiburudika kwa kuangalia michezo mbalimbali kwenye televisheni na muziki mororo.

**Afya bora ndiyo mtaji mkubwa katika maisha. Wasiliana nasi kwa namba ya simu: 0748 109 109**

***Chagua Kitonga Farm, Chagua Afya Njema.***

## Wanasheria

### TLS yahadhari, yatoa ushauri

#### Inatoka Uk. 10

usalama, masuala ya ajira na yaliyomo ya ndani, masuala ya kodi, mahitaji ya kiufundi, vibali vya serikali, haki za upyaishaji wa vibali au leseni, au dhidi ya kusimamishwa au kufutwa kwa vibali au leseni. Kampuni ya Mradi haiwezi kuwa chini ya sheria za Tanzania na sheria ya Kiingereza kwa masuala sawa.

2.3.3. Mapendekezo ya TLS: TLS inapendekeza Kifungu cha 21 kifanyiwe marekebisho kwa sababu zilizotajwa hapo juu. Kifungu cha 21 kinapaswa kusema kuwa IGA inaongozwa na Sheria ya Tanzania. Hii inaweza kufanikiwa kupitia Kifungu cha 22 cha IGA, mara baada ya mchakato wa kuridhia kukamilika kwa kubadilishana vyombo vya kuridhia kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 25 (4).

2.3.4. Msingi wa Mapendekezo ya TLS: IGA inasema kuwa sheria zinazotumika ni Sheria ya Kiingereza na Sheria za Tanzania, ambayo inaleta suala kwa sababu mkataba haujafanua kikomo au wigo wa matumizi ya sheria hizi. Mkataba unatoa haki kwa pande zote kuhusu Haki za Ardhi.

Kwa kuzingatia hili, Sheria ya Kiingereza na sheria za Tanzania zinatofautiana kuhusu suala hili—nchini Tanzania, mgeni hawezi kumiliki ardhi kama ilivyoelezwa na Sheria ya Ardhi, isipokuwa mgeni anamiliki ardhi kwa madhumuni ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (kama ilivyoainishwa na Sheria ya Ardhi na Sheria ya Uwekezaji) kifungu cha 20 (1) cha Sheria ya Ardhi Cap 113 RE 2019 na Kifungu cha 17 (2) cha Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania Cap 26 ya 1997 RE 2019. Kwa upande mwingine, sheria ya Kiingereza haiweki vizuizi sawa kwa wageni kumiliki ardhi kama ilivyo katika Tanzania.

2.3.5. Kutarajia Athari ya suala kwa Nchi Yetu: Ikiwa kifungu hiki kitabaki bila kufanyiwa marekebisho, kinaweza kusababisha mgongano wa sheria zinazotumika, ambapo IGA, kama mfumo

wa kivuli, utatawaliwa na sheria tofauti na HGAs. Kutumia sheria ya Kiingereza kwa masuala kama haki za ardhi, motisha za uwekezaji, mazingira na afya ya kazi, haki za kazi, usalama na haki za usalama nchini Tanzania haitawezekana. Kampuni ya Mradi haiwezi kutawaliwa na sheria za Tanzania na Kiingereza kwa masuala sawa.

#### 2.4 MAREKEBISHO YA IGA

2.4.1 Kifungu: Kifungu cha 22 cha IGA kinabainisha kuwa marekebisho kwa IGA yanaweza kufanywa wakati wowote kwa maandishi kupitia makubaliano ya pande zote. Aidha, inathibitisha kuwa hakuna marekebisho yatakayofanyika bila makubaliano, yaliyothibitishwa kwa saina na uthibitisho na / au kupitishwa kwa hati sahihi, na pande zote za Serikali.

2.4.2 Uchunguzi wa TLS: TLS inaona kuwa IGA inatoa marekebisho kupitia Kifungu cha 22. Walakini, kifungu hiki kinaamuru kwa kawaida kuwa marekebisho yanaweza kupendekezwa tu baada ya IGA kupitishwa na hati za uthibitisho zimebadilishwa. IGA inakuwa halali tu baada ya kubadilishana kwa hati za uthibitisho (Kifungu cha 31).

TLS inaona kuwa ni ajabu na hatari sana kwamba IGA inaruhusu pande kufanya marekebisho baada ya tukio. Kifungu cha 22 pia hakizungumzii wakati wa maamuzi juu ya marekebisho ya IGA. Mkataba unapaswa kuainisha wakati, baada ya kupokea pendekezo la marekebisho na pande zote kukubaliana na kuanzisha ratiba ya kusindika na kuchukua hatua za mwisho kwa pendekezo la marekebisho.

2.4.3 Mapendekezo ya TLS: Kwa kuzingatia umuhimu na ukubwa wa kasoro na maeneo yanayohitaji marekebisho kama yaliyoelezwa katika hati hii, TLS inapendekeza kwamba Serikali ya Tanzania itumie mara moja Kifungu cha 22 kushughulikia masuala hayo. Kifungu cha 22 pia kinapaswa kufanyiwa marekebisho ili kujumuisha

## **TLS yahadhari, yatoa ushauri**

ratiba ya maamuzi juu ya marekebisho ya IGA. TLS inapendekeza kuwa jumla ya kipindi cha pande zote kukubaliana na kuanzisha ratiba ya kusindika na kumaliza pendekezo la marekebisho haitazidi siku 30.

2.4.4 Msingi wa Mapendekezo ya TLS: Uzito, ukali na umuhimu wa kasoro zilizotambuliwa katika vipengele mbalimbali vya IGA kama ilivyoelezwa katika taarifa hii.

2.4.5 Athari Inayotarajiwa kwa Nchi Yetu: Ikiwa vipengele na kasoro hazitafanyiwa marekebisho, TLS ina wasiwasi kuwa IGA itatekelezwa licha ya kasoro zake. Mara baada ya kupitishwa, IGA inakuwa inabana pande, na marekebisho yanaweza kufanikiwa ikiwa pande zinakubaliana. Vinginevyo, IGA itatekelezwa kama ilivyopitishwa, kwa uwezekano wa kudhuru upande ulioathirika.

### **2.5 MUDA NA HITIMISHO LA MKATABA**

2.5.1. Vifungu: Kifungu cha 23 (1) kinabainisha hali mbili za kusitisha: (i) kusitisha kabisa shughuli zote za Mradi; au (ii) kumalizika kwa HGAs zote na Mikataba ya Mradi (ikiwa ni pamoja na nyongeza au muda wa ziada) na ufumbuzi wa migogoro, ikiwa ipo. Aidha, Kifungu cha 23 (2) kinashughulikia kesi ambapo HGA inasitishwa mapema, na kupendekeza kuongeza makubaliano hayo ili kuruhusu chama au Kampuni ya Mradi kulinda haki zake. Kifungu cha 23 (3) kinabainisha kuwa IGA haiwezi kusitishwa bila ridhaa ya chama kingine, ambayo haipaswi kukataliwa kwa sababu zisizo za msingi. Kifungu cha 23 (4) kinatangaza kuwa Nchi Haziwezi kutoa taarifa, kujiondoa, kusimamisha, au kusitisha Mikataba huu chini ya hali yoyote, ikiwa ni pamoja na uvunjaji wa msingi, mabadiliko makubwa ya hali, kuvunja uhusiano wa kidiplomasia au konsulari, au sababu nyingine yoyote inayotambuliwa chini ya sheria za kimataifa. Walakini, migogoro yoyote

inayotokea chini ya hali hizo kati ya Nchi Haziwezi kushughulikiwa kulingana na maelekezo ya Kifungu cha 20 cha Mkataba huu.

2.5.2. Mapendekezo ya TLS: Kifungu cha 23 (1) cha IGA, ambacho kinahusisha muda wa mkataba na uwepo wa uwekezaji unaohusiana, ni kawaida kwa mkataba wa uwekezaji kama IGA, na inamaanisha vizuizi vya kusitisha. Mikataba ya Uwekezaji wa Kibilateral (BITS) mara nyingi ina muda maalum unaoweza kufutwa. Ikiwa kuna muda uliowekwa, mwekezaji atalenga kuweka kifungu kinachounganisha mkataba zaidi ya tarehe ya kumalizika kwa uwekezaji wa sasa ikiwa mkataba hautafutwa.

TLS ina maswali kwa nini Kifungu cha 23 (2), ambacho kinashughulikia HGA kusitishwa mapema, hakiwezi kuondolewa kutoka kwa IGA na badala yake kuingizwa kwenye HGAs. TLS ina wasiwasi mkubwa juu ya Kifungu cha 23 (3), ambacho kinabainisha kuwa IGA haiwezi kusitishwa bila ridhaa ya chama kingine. Aina hii ya kufunga inaweza kusababisha madhara kwa chama kinachotaka kumaliza mkataba. Ingawa IGA inataja kuwa chama hakitakataa ridhaa kwa sababu zisizo za msingi, hii inaweza kuwa na madhara ambapo IGA inaweka vizuizi vya kusitisha hata katika kesi ya uvunjaji mkubwa wa msingi. TLS inaamini kuwa kifungu hiki hakiendani na maslahi ya Tanzania au mchakato wa ufumbuzi wa migogoro.

Zaidi ya hayo, TLS inachukulia Kifungu cha 23 (4), ambacho kinazuia Nchi Haziwezi kutoa taarifa, kujiondoa, kusimamisha, au kusitisha Mikataba huu chini ya hali yoyote, kama sio sahihi na inayopendelea upande mmoja. Ikiwa kuna uvunjaji mkubwa wa msingi, Tanzania haitaweza kusitisha IGA isipokuwa kupitia Kifungu cha 23 (3), ambacho kinahitaji ridhaa ya chama kingine. Vifungu vya 23 (3) na 23 (4) ni nadra sana kwa sababu vinazuia hatua

## Wanasheria

### TLS yahadhari, yatoa ushauri

za marekebisho. Walakini, inaruhusu usuluhishi ikiwa kuna mgogoro, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 20, ingawa mchakato huu ni mrefu sana.

2.5.3. Mapendekezo ya TLS: Inapendekezwa sana kwamba IGA ya Kifungu 23(3) na 23(4) iondolewe kabisa. Aidha, TLS inapendekeza kwamba IGA iwe na vipengele vya Kifungu 23(1) na 23(2) tu. Mkataba, ulioingwiwa kwa hiari na pande zote, unapaswa kuruhusu pande yoyote kuvunja mkataba huo, kwa sharti kwamba taarifa ya awali imepatikana kwa pande zote.

TLS inapendekeza kipindi cha taarifa ya siku 30 au zaidi kwa ajili ya kuvunja mkataba. Zaidi ya hayo, maneno katika Kifungu 23(1), “kukoma kwa shughuli zote za mradi” au “kumalizika kwa HGA zote na makubaliano yote ya mradi na ufumbuzi wa migogoro,” ni pana sana na inapaswa kufikiriwa upya kwa maslahi ya pande zote.

2.5.4. Msingi wa Mapendekezo ya TLS: Tanzania ni mwanachama na mdau wa Mkataba wa Haki na Majukumu ya Kiuchumi ya Mataifa, lengo kuu la Tanzania ni kukuza utaratibu mpya wa kiuchumi wa kimataifa uliojengwa juu ya usawa, usawa wa kujitawala, utegemezi, maslahi ya pamoja, na ushirikiano kati ya mataifa yote, bila kujali mifumo yao ya kiuchumi na kijamii.

Kifungu cha 2(2) kinawezesha kila nchi kusimamia uwekezaji wa kigeni ndani wa mamlaka yake ya kitaifa kulingana na sheria, kanuni, malengo, na vipaumbele vyake. Vipengele vya IGA havipaswi kufasiriwa kuzuia haki za Tanzania kusimamia au, katika hali mbaya zaidi—kujiondoa au kukataa mkataba kwa njia inayofaa na sheria zake za ndani na za kimataifa.

2.5.5. Athari Inayotarajiwa ya Suala Hili kwa Nchi Yetu: Ikiwa kifungu hiki hakitabadilishwa, chama kimoja kinaweza kutumia vipengele vya IGA kufanya kuvunja mkataba kuwa haiwezekani. Mkataba wa kudumu, licha ya uvunjaji wa

vifungu, mabadiliko muhimu ya hali, au kuvunjika kwa uhusiano wa kidiplomasia, unaweka hatari kwa maslahi ya Jamhuri ya Muungano na watu wake.

2.6 UFAULU KABLA YA MKATABA NA UTEKELEZAJI

2.6.1. Kifungu: Kifungu cha 25(1) kinawalazimisha Tanzania kutekeleza “hatua za utawala na uhibititi baada ya kusaini IGA ili kuhakikisha kuwa ‘Shughuli za Awali za Mradi’ zinaweza kufanywa kisheria na/au kwa niaba ya mwekezaji mmoja au zaidi au Kampuni ya Mradi.” Shughuli za Awali za Mradi zinatambuliwa katika Kifungu cha 1 cha IGA kama shughuli yoyote ya Mradi iliyoizinduliwa kabla ya uamuzi wa uwekezaji wa mwisho kuhusu Mradi, haswa kazi za kiufundi muhimu kwa kubuni mbele ya mfumo unaohusiana na hatua ya awali ya kubuni, ujenzi, na maendeleo.

2.6.2. Uchunguzi wa TLS: Gharama za Shughuli za Awali za Mradi na hatari ya dhima kwa chama mwenyeji ikiwa uthibitisho utakataliwa inaweza kuwa kubwa. Kifungu cha 25(1) kinathibitisha mikataba kwa Shughuli za Awali za Mradi zilizofanywa kabla ya uthibitisho chini ya IGA. Haijulikani ikiwa Shughuli za Awali za Mradi wowote zimefanyika chini ya IGA. Ni nadra kwa makubaliano, ambayo yanahitaji uthibitisho, kuwa na kifungu kikubwa ndani yake kinachofanya kazi kabla ya makubaliano kuthibitishwa.

2.6.3. Mapendekezo ya TLS: TLS inapendekeza kuondoa marejeleo yote kwa shughuli za awali za mradi kutoka kwa IGA. TLS inaamini kuna hati ya kisheria iliyopo inayosimamia shughuli za awali za mradi, ambayo inapaswa kuwa ya kisheria na ya kujitolea.

2.6.4. Msingi wa Mapendekezo ya TLS: Ni nadra kwa makubaliano, ambayo yanahitaji uthibitisho, kuwa na kifungu kikubwa ndani yake kinachofanya kazi kabla ya makubaliano kuthibitishwa.

Kwa kuwa IGA inatumia mara kwa

## **TLS yahadhari, yatoa ushauri**

mara neno “nchi washirika”, TLS inataka kurejelea Ibara 12 (2) (b), 10, na 18 ya Mkataba wa Vienna juu ya Sheria ya Mikataba ya 1969:

Mwakilishi anaweza kusaini mkataba ad referendum, maana yake saina hiyo ni halali tu baada ya kuthibitishwa na nchi yake. Katika kesi hii, saina hiyo inakuwa ya mwisho wakati inathibitishwa na mamlaka husika—katika muktadha huu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<sup>3</sup>

Zaidi ya hayo, ambapo saina inategemea uthibitisho, kukubalika, au idhini, haiwezi kuanzisha ridhaa ya kufungwa. Badala yake, ni njia ya uthibitisho na inawasilisha nia ya nchi inayosaini kuendelea na mchakato wa kutengeneza mkataba. Saina inakidhi hali ya nchi inayosaini kuendelea na uthibitisho, kukubalika, au idhini. Pia inaunda wajibu wa kujizuia, kwa nia njema, kutoka kwa hatua ambazo zingeweza kudhoofisha malengo na madhumuni ya mkataba.<sup>4</sup>

2.6.5. Athari Inayotarajiwa ya Shida kwa Nchi Yetu: Kufanya kifungu kikubwa katika IGA kifanye kazi kabla ya makubaliano kuthibitishwa kunaweka wajibu kwa Nchi. Zaidi ya hayo, kuruhusu kuanzisha utekelezaji wa sehemu ya IGA (Shughuli za Awali za Mradi) bila makubaliano maalum ya mradi inaweza kuifanya nchi yetu iwe katika hatari ya migogoro isiyo ya lazima ya uwekezaji na hasara inayowezekana.

Pia, inanyima Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nafasi ya kuzuia, kwa nia njema, hatua ambazo zingeweza kudhoofisha malengo na madhumuni ya IGA.

### **2.7 AHADI YA KUTOKUWA NA MGOGORO (HAKI ZA PARTIES KUJIHUSISHA NA MAJUKUMU YA KIMATAIFA NA YA NDANI)**

2.7.1. Kifungu: Kifungu cha 27 kinabainisha kwamba kila nchi mshiriki inahakikisha na kuthibitisha kwamba, baada ya makubaliano haya kuanza kutumika na sheria zote zinazohusiana,

haitashiriki katika makubaliano yoyote ya ndani au ya kimataifa au majukumu, au kuwa na wajibu wa kisheria wa kuzingatia au kutekeleza sheria, kanuni, au makubaliano ya ndani au ya kimataifa, ambayo yanapingana au kutekeleza makubaliano haya au HGA husika na Mkataba wowote wa Mradi ambao Nchi Mshiriki huyo ni mshiriki.

2.7.2. Uchunguzi wa TLS: Tunagundua kwamba wajibu wa kutokuwa na mgogoro unahusisha HGAs na Mkataba wa Mradi wa baadaye. Kifungu cha 27 cha IGA kinawajibisha Tanzania hasa kutokuwa sehemu ya makubaliano yoyote ya ndani au ya kimataifa au majukumu, au kuwa na wajibu wa kisheria wa kuzingatia au kutekeleza sheria, kanuni, au makubaliano ya ndani au ya kimataifa, ambayo yanapingana au kuanzisha au kutekeleza Mkataba husika au HGA husika na Mkataba wowote wa Mradi ambao Nchi Mshiriki huyo ni mshiriki.

2.7.3. Mapendekezo ya TLS: TLS inapendekeza kubadilisha Kifungu cha 27 ili kikomeshe wajibu wa kutokuwa na mgogoro tu kwa IGA kwa sababu lengo la wajibu wa kutokuwa na mgogoro ni kuhakikisha kwamba pande zinazofanya makubaliano zinaweka wazi majukumu ya kisheria au ya kisheria ambayo yanaweza kuzuia au kuzuia chama kinachofanya ahadi kutimiza majukumu yake chini ya makubaliano mara baada ya makubaliano hayo kukamilika na kuanza kutumika.

2.7.4. Msingi wa Mapendekezo ya TLS: Upeo wa Kifungu cha 27 haupokezi kwa sababu unapanua wajibu kwa HGAs na Mkataba wa Mradi wa baadaye. Hii inaleta masuala kwa sababu inawezekana kuifanya Tanzania iwe na dhima kwa uvunjaji usio wa makusudi wa Kifungu cha 27.

HGAs na Mkataba wa Mradi utajumuisha vifungu vinavyoshughulikia kutokuwa na mgogoro. Hakuna haja ya kuongeza wajibu wa kutokuwa na



## Tangazo

# Tangaza na Pambazuko

EWE mfanyabiashara na mtoa huduma, endapo unahitaji kuwafikia wateja wengi zaidi bila kujali mipaka ya eneo ulilopo, tangaza nasi

Pambazuko isaidie kupaisha na kupambazua huduma na biashara yako.



*Kwa bei nafuu sana*

0744 768 263 au Barua-  
Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)

## Hata hili la bandari tunaweza

Na Makoye KISENAH

**K**AMA ni hoja katika malumbano kuhusu mkataba wa ushirikiano baina ya Tanzania na Dubai, unaofungua mlango kwa kampuni ya DP World ya Dubai kuja kuingia makubaliano na Mamlaka ya Uendeshaji wa Bandari Tanzania (TPA), tumezisikia sana.

Tumesikia hoja za wanaounga mkono hatua hiyo ya serikali na sababu zao kwa nini hatua hiyo inapaswa kuchukuliwa sasa. Kwa upande mwingine, tumezisikia hoja za wanaopinga, wakikosoa baadhi ya vifungu katika mkataba huo na kutuaminisha kuwa Tanzania haipaswi kukumbatia makubaliano hayo kwa kuwa vipo baadhi ya vifungu vinavyoonyesha “nchi itakuwa imepigwa.”

Jambo ambalo halijasikika kwa kiasi kikubwa ni nini kifuata baada ya malumbano hayo.

Wakati wale wanaounga mkono hatua hii wakisema hakuna kibaya chochote kwenye mkataba, hivyo mchakato unaweza kuendelea, wale wanaopinga wanasema upo umuhimu wa kurekebisha kwanza baadhi ya vifungu kwenye mkataba kabla ya uamuzi wa kuikaribisha DP World kuendesha bandari haujafikiwa.

Kimsingi, pande hizi mbili zinakubaliana kuwa uwekezaji katika bandari nchini ni suala linalohitajika sana

kwa ajili ya maendeleo. Kinachobishaniwa ni baadhi ya vifungu vya mkataba tu na siyo mkataba wote.

Ingawa lipo kundi la watu wanaosema kuwa matatizo katika vifungu hivyo vichache, kutokana na nguvu zake kisheria, vinaufanya mkataba mzima kuwa mbaya na hivyo mkataba huo ufutwe kwa ujumla wake.

Lakini, hao nao pia wanakubali kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kufanya uwekezaji kwenye bandari nchini.


Nadhani hapo kwenye suala la uwekezaji kwenye bandari ndipo penye mzizi wa suala hili kwa wakati huu ambapo mijadala hii inaonekana kuishiwa na hoja mpya.

Kitu kikubwa ambacho tunapaswa kukiangalia kama Watanzania ni uwekezaji kwenye bandari zetu, hasa bandari ya Dar es Salaam, ambayo inashughulikia asilimia 90 ya shehena yote nchini inayosafirishwa nje, unatupa manufaa tunayoyatarajia kutoka katika miundombinu hiyo.

Bandari hii ndilo langu kuu, siyo nchini tu, bali hata kwa baadhi ya nchi zinazotuzunguka kama vile Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Uganda, Burundi, Malawi na Rwanda. Hivyo, umuhimu wake unapindukia mipaka ya nchi.

Kama makundi mengi katika malumbano haya yanakubaliana kuwa

*Endelea Uk. 18*



Sehemu ya Bandari ya Dar es Salaam

**Makala****Hata hili la bandari tunaweza***Inatoka Uk. 17*

uwekezaji kwenye bandari ni suala muhimu, nadhani ni vyema sasa tukajikita kulijadili hilo kwani tutakuwa tunapiga hatua zaidi kuelekea mbele.

Kuendelea kubishana kuhusu vifungu vya mkataba kutatufanya tubaki kulekule kwenye hatua ya kwanza, tutazidi kupoteza muda zaidi.

Kwa kuwa pande zote zinazopingana kuhusiana na suala hili wanakubaliana kimsingi kuwa uwekezaji katika bandari ni jambo muhimu, ni vyema pia mjadala ukaelekezwa kwenye namna bora ya serikali kuimarisha bandari kupitia uwekezaji, kuliko kuendelea mjadala wa vifungu vya mkataba ambao imeonyesha kutokuwa na tija kubwa sana.

Na katika uwekezaji huo, kwa kuwa baadhi ya watu wameshaonyesha wasiwasi kuhusiana na kampuni ya DP World, ingawa serikali imeonyesha kuwa matarajio yake makubwa ya kuimarisha bandari ni kupitia kampuni hiyo, ni vyema hivi sasa tukawa na mawazo kuhusu namna mbadala ya kuwekeza katika bandari bila ya kulazimika kuwa na malumbano mengine ambayo yatazidi kutupotezea muda.

Wakati malumbano haya yakiendelea, serikali imekuwa ikijinasibu kuhusu miradi mikubwa ya reli ya kisasa (SGR), kufufua Kampuni ya Ndege (ATCL) na ujenzi wa bwawa kubwa la kuzalisha umeme kwa njia ya maji la Julius Nyerere (JNHPP).

Miradi yote hii mikubwa tumekuwa tukielezwa kwamba imegharamiwa na serikali yenyewe, iwe kwa kupitia kutenga fedha zake kwenye bajeti moja kwa moja au kupitia mikopo.

Ingawa miradi hii mikubwa haijakamilika kwa asilimia 100, lakini maendeleo yake yanaonyesha mafanikio makubwa. Kwa hatua iliyofikia, pamoja na baadhi ya kasoro zilizojitokeza, imeonyesha kuwa kuna jambo ambalo serikali inaweza kujifunza kutoka kwenye miradi hiyo.

Moja ya jambo ambalo linaweza kutupatia funzo kama taifa ni jinsi miradi hiyo ilivyotekelezwa kwa ufanisi kwa kutumia fedha zetu wenyewe.

Mathalan, ujenzi wa JNHPP unagarimu zaidi ya Sh6.5 trilioni huku ujenzi wa SGR ukiharimu zaidi ya Sh2.5 trilioni. Ukijumuisha na ufufuaji wa ATCL unaweza kuona kuwa nchi inetumia takribani Sh10 trilioni kwa ajili ya miradi hii mikubwa mitatu.

Wakati serikali ya awamu ya tano ilipotangaza kuanza ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa kutumia fedha za ndani, kutokana na gharama zake kuwa kubwa, baadhi ya watu walipinga kutumia fedha za ndani wakiishauri serikali kutafuta namna nyingine ya kutekeleza mradi huo ikiwamo kuishirikisha sekta binafsi.

Hata lilipokuja suala la kutumia fedha za bajeti kununua ndege mpya kwa ajili

*Endelea Uk. 19*

**Ndege mali ya Serikali ya Tanzania**

## Hata hili la bandari tunaweza

*Inatoka Uk. 18*

ya ATCL, baadhi ya wachumi waliishauri serikali kukopa ndege hizo.

Hapa, jambo la msingi ni kuwa serikali ilishafikia uamuzi wa kufanya hayo iliyoikusudia kuyafanya. Ushauri uliokuwa unatolewa au upinzani ulikuwepo kwenye namna ya kutekeleza suala hilo.

Ingawa baadhi ya wachumi walipendekeza njia nyingine ya kutekeleza miradi hiyo, lakini serikali ikabaki na mpango wake uleule wa kutumia fedha zake kugharamia miradi hiyo. Leo hii matokeo yake yanaonekana.

Ujenzi wa SGR unakwenda vizuri (pamoja na matatizo ya hapa na pale yanayojitokeza), ufufuaji wa ATCL nao umefikia pazuri kwani sasa kwa suala la uhakika wa safari siyo tena kikwazo kwani kampuni ina ndege za kutosha.

Kuhusu Bwawa la Julius Nyerere, sasa tunasubiri kukamilika kufungwa kwa mitambo tu ili uzalishaji wa umeme uanze, kwani tumeshatangaziwa kuwa kina cha maji kimefikia kiwango ambacho kinaruhusu kazi ya kufua umeme kuanza.

Ni dhahiri kuwa kwa hatua zilizobakia serikali haitashindwa kukamilisha utekelezaji wa miradi hii mikubwa. Suala la kujiuliza hapo ni kuwa iwapo serikali iliweza kutekeleza miradi hii mikubwa mitatu bila kuhitaji uwekezaji au ufadhili kutoka nje, inashindwaje kuendeleza bandari kwa kiwango kinachotakiwa kwa kutumia rasilimali za ndani ili iwe na ufanisi unaohitajika bila kuhitaji mkono wa mshirika kutoka nje?

Kwa kuwa baadhi ya watu wameonyesha wasiwasi kuhusiana na mpango huu wa kuimarisha bandari kwa kuitumia kampuni ya DP World, ni vyema serikali ikaja na mpango mwingine utakaohusisha serikali kutumia fedha zake yenyewe ili kuiendeleza bandari.

Ni wakati sasa wa serikali kuja na mpango wa kuimarisha shughuli za bandari kwa kuwekeza fedha zake yenyewe. Hakuna haja ya kuwa na hofu kuwa inaweza kushindwa kufanya hivyo



*Sehemu ya Bwawa la Julius Nyerere*

kwa sababu miradi mikubwa mitatu iliyoitekeleza kwa ufanisi inaonyesha kuwa serikali inaweza kufanya hivyo.

Hatupaswi kuwa na hofu kuwa serikali inaweza kukosa teknolojia bora ya kubadilisha miundombinu ya bandari. Kama tukiwa na fedha tutaweza kuitumia kampuni yoyote kutufanyia kazi hiyo kama ambavyo tumezitumia kampuni ya Misri na Uturuki kutujengea bwawa la Nyerere na SGR.

Kama tuliweza kupata takribani Sh10 trilion kwa ajili ya kuendeleza miradi mikubwa mitatu ambayo inaonyesha mafanikio makubwa, ni dhahiri kuwa hatutaweza kukosa fedha kwa ajili ya kuendeleza bandari zetu, eneo ambalo linatajwa kama kitovu cha mapato ya nchi na lango kuu la biashara kwa Tanzania na mataifa yanayotuzunguka.

Badala ya kulumbana sisi kwa sisi kuhusu nani anastahili kukaribishwa kuleta mapinduzi katika utendaji wa bandari, ni wakati wa serikali sasa kuchukua hatamu ya jambo hilo na kulitekeleza kwa namna ileile iliyotumika kuendeleza miradi mingine mikubwa ya SGR, ATCL na JNHPP

## KIKWETE NA WAHADZABE



Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete akimsikiliza mwananchi kutoka jamii ya Wahadzabe (katikati) wakati akijibu swali aliloulizwa na Mbunge wa Mchinga, Salma Kikwete. Rais Kikwete na mkewe, Salma walikuwa na ziara ya kutembelea jamii hiyo hivi karibuni katika Kijiji cha Endamagha kilichopo Kata Tarafa ya Eyasi, Wilaya ya Karatu, Arusha. (Picha na mitandao).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

